

# MRADI SHIRIKISHI WA MAENDELEO YA BARABARA NA UTUMIAJI WA FURSA ZA KIJAMII NA KIUCHUMI

## Mwaliko kwa Umma Kushiriki katika Jukwaa la Mashauriano Litakalofanyika Mtandanoni kutambulisha Mradi pamoja na Nyaraka za Mfumo wa Kimazingira na Kijamii Zinazohusu Mradi huu

Serikali ya Tanzania, kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Wakala wa Barabara nchini Tanzania (TANROADS) kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, inaandaa Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Barabara katika Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE). Lengo la mradi huu ni **“kuboresha upitikaji wa barabara za vijijini katika maeneo yaliyoteuliwa na kujenga uwezo katika usimamizi endelevu wa barabara za vijijini kwa kuishirikisha jamii”**.

Mradi huu utatekelezwa katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Kusini na Pwani ya Tanzania Bara. Lengo lake ni kuimarisha taasisi katika kushughulikia maeneo mahususi, kutunza barabara, kuishirikisha jamii na kuyafanyia kazi masuala yanayohitaji shughuli za dharura. Mradi utahusisha ujenzi wa barabara katika halmashauri tatu za wilaya katika Mkoa wa Iringa ambazo ni Kilolo, Iringa Vijijini na Mufindi.

Nyaraka zote muhimu za mifumo inayohusu usimamizi wa kimazingira na kijamii zimeshaandaliwa. Nyaraka hizi ni pamoja na: Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii, Mfumo wa Sera ya Uhamishaji mali zinazo athiriwa na mradi, Mpango wa Usimamizi wa Masuala ya Kimazingira na Kijamii, Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau, Mfumo unaohusu Taratibu za Usimamizi wa wafanyakazi na Mipango ya Makundi Hatarishi.

TARURA inawaalika wadau wote kuhudhuria Jukwaa la Mashauriano litakalofanyika tarehe 2 Aprili, 2020 kuanzia saa 3:00 asubuhi. Kwa bahati mbaya, kutokana na tishio la kuenea kwa Virusi vya Korona, mashauriano hayo yatafanyika kwa kutumia mtandao, yaani kutumia programu ya Webinar inayowawezesha wadau kufanya mkutano kwa kutumia intaneti.

Lengo la mkutano huu ni kuutamulisha Mradi shirikishi wa Maendeleo ya Barabara na Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE) na nyaraka za mfumo wa kimazingira na kijamii zinazohusu mradi huu kwa umma na wadau wote na kukusanya maoni kwa ajili ya kuuboresha.

Ili kuufuatilia Mkutano huo wa Jukwaa la Mashauriano pamoja na mawasilisho, tumia anwani ya mtandao (webinar) <https://www.tarura.go.tz/index.php/roads-inclusion-and-socioeconomic-opportunities-program-rise> itakayopatikana kuanzia tarehe 1 Aprili, 2020.

Taarifa zote za msingi kuhusu Mpango wa Ushirikishaji wa Maendeleo ya Barabara na Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE), nyaraka zinazohusu Mfumo wa Kimazingira na Kijamii pamoja na mihutasari yake katika lugha za Kiingereza na Kiswahili zinapatikana katika tovuti zifuatazo za TARURA na TANROADS: [tarura.go.tz](http://tarura.go.tz) na [tanroads.go.tz](http://tanroads.go.tz) Nakala ngumu za nyaraka hizo zitapatikana katika ofisi zote za Waratibu wa Mikoa na Mameneja wa Halmashauri.

Umma na wadau wote ambao wanatarajia kuwasilisha maoni yao kwa maandishi katika Mradi shirikishi wa Maendeleo ya Barabara na Utumiaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi (RISE) wanaalikwa kufanya hivyo kwa kutumia anwani iliyoopo hapa chini:

Mtendaji Mkuu,  
Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini,  
S.L.P. 11042  
Jengo la PSSSF, Ghorofa ya 8, Barabara ya UDOM,  
Dodoma, Tanzania  
Baruapepe: [ceo@tarura.go.tz](mailto:ceo@tarura.go.tz)  
Simu: +255745810140